KARATASI YA UKWELI

Kuwa kwenya mahusiano na watu walio kuzidi umri

Maelezo muhimu

Mwaise anafikiria kuwa kwenye mahusiano na mtu aliye mzidi umri lakini hana uhakika.
Je, nini anapaswa kufanya?

Kuwa na mahusiano na mwanaume au mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi kuliko wewe – Inawezekana unapewa zawadi nyingi na unapelekwa sehemu za kifahari lakini kumbuka:

- **Wanaweza kutegemea au kulazimisha uwapatie vitu usivyotaka kuwapatia, kama kufanyka mapenzi.**
- **Kunauwezekano mkubwa kwamba watataka kusikilizwa wao tu, kwa hiyo itakuwa vigumu kwako kuzungumzia kuhusu matumizi ya kondomu.**
- **Kuna uwezekano mkubwa kwamba wanaweza wakawa wanaishi na virusi vya ukimwi. Kama hutakubali kutumia kondomu basi utajiweka kwenye hatari ya kupata virusi vya ukimwi na magonjwa mengine ya ngono.**
- **Wanaweza wakawa wanafanya ngono na watu wengine wenye umri kama wako, hii huongeza hatari ya maambukizi zaidi ya magonjwa ya ngono.**
- **Unaweza hisi ukotayari, lakini matarajio yao yanaweza yakawa tofauti na yako.**
- **Kwakuwa marafiki zako wanamahusiano na watu wazima, bado utapaswa kufanya maamuzi sahihi.**

Mawazo ya mjadala

Ni nini ambacho wewe au kikundi chako mnafikiria kuhusu mahusiano ya watu wenye umri tofauti kabisa? Labda hujawahi kulifikiria hili kabla. Haya ni maswali ya kufikiria binafi au kujadili kwenye kikundi chako.

- **“Blessers” ni mfano wa jina ambalo hupewa mwanaume anaye toka na wasichana wado sana kumliko, “Ben 10’s” nimfani wa jina analipewa kijana mdogo anaye toka na wamama wenye umri mkubwa kumliko. Je kunamajina mengine ambayo hutumuka mahali unapoishi? Unaposikia watu wakiitwa majina haya, inakupa mtazamo gani?**

- **Unadhani ni sababu gani ambazo hufanya vijana wa kike na vijana wa kiume kuwa kwenye mahusiano na watu wazima?**
- **Kma ungekuwa unatoka na mtu aliye kuzidi umri ambaye anakupatia msaada wa kifedha, unadhani hili lingeathiri vipi mahusiano yako? Fikiria kuhusu faida na hasara ambazo zinaweza kupatikana.**
- **Je, unafahamu kwamba wanaume na wanawake wazee wanauwezekano mkubwa zaidi wa kuwa na VVU au magonjwa mengine ya ngono kuliko vijana, kwasababu wamekuwa wakifanya mapenzi kwa muda mrefu? Je, hili linaweza kubadilisha mtazamo wako kuhusu kutoka na watu walio kuzidi umri Zaidi?**
- **Mahusiano ya wengi ambao wametofautiana miaka, ni yale ya watu ambao hawakufunga ndoa. Unadhani nini kinaweza kuwapata vijana wadogo walio kwenya mahusiano ya aina hii?**

Habari Zaidi

Ishara za maonyo ya mahusiano yasiyo salama
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/martha

Jinsi ya kukataa kufanya ngono
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/chipo

Kuongelea kuhusu virusi vya ukimwi na mwenzi wako
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/lineo

Ngono bila kondomu
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/spijo

Njia mbalimbali za uzazi wa mpango
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/babalwa

Young Voices ni kikundi kinacho jadili kuhusu mijadala mbalimbali ya afya ya uzazi na kufanya ngono salama. Unaweza kupata taarifa za kutosha kwenye: **https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/**

March 2021